ALPHA HABARI

Toleo la Januari

*31 januari, 2026*

Mawasiliano kuchochea mageuzi chanya ya kampuni ya Alpha UK 5



**Dkt. Massaga "Majukwaa ya kidijitali kukuza uchumi wa Tanzania" UK 6**

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

**TRA mguu sawa kuzindua mfumo wa IDRAS UK 3**

# Alpha yajipanga kutumia mfumo wa IDRAS kikamilifu

Kuanzia tarehe 15 hadi 17 Januari 2026, wafanyakazi wa Alpha Associates Tanzania LTD tawi la Dar es Salaam walipata nafasi ya kuhudhuria mafunzo ya mfumo Jumuishi wa Utawala wa Mapato ya Ndani (IDRAS),yaliondaliwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) jijini Dar es Salaam katika ukumbi wa mikutano wa Mlimani City. **UK 2**





**Dkt. Massaga ahaidi makubwa 2026. UK 1**





**NEEC kuboresha mazingira wezeshi kwa wajasiriamali vijana. UK 15**

**VIPAUMBELE VYA DIRA YA TAIFA 2025/2050 UK 10**




**JUKWAA LA UWEKEZAJI NA FURSA ZA KIUCHUMI NCHINI UK 13**

- **ijue kodi ya mapato kwa makampuni na watu binafsi Nchini Tanzania. UK 4**
- **Yajue makosa ya kawaida ya kodi kwa Biashara Ndogo na za Kati na jinsi ya kuyaepuka au kuyakwepa kisheria UK 11**
- **ijue kodi ya ongezeko la thamani (vat) kwa undani zaidi Nchini Tanzania UK 14**
- **Zijue, haki na wajibu wa mlipa kodi chini ya sheria za kodi Nchini Tanzania UK 16**

**Jishindie Zawadi kwa kujibu Maswali ya kikodi UK 18**

UK 8 Jarida Madhubuti lenye lengo la kutoa Elimu ya Kodi na Biashara limetolewa na Alpha Associates Tanzania Limited

# ALPHA HABARI

Toleo la Januari

*31 januari, 2026*

**ARUSHA.**



**Dkt. Alphonce Dotto Massaga**
Mkurungenzi Alpha associates Tanzania Ltd

## Dkt. Massaga ahaidi makubwa 2026.

Tarehe 5 Januari 2026, Mkurugenzi Mtendaji wa Alpha Associates Tanzania LTD, Dkt. Alphonce Dotto Massaga, alihutubia hotuba yake ya kwanza ya mwaka 2026 kwa wafanyakazi wa Alpha Associates

Akizungumza wakati wa mkutano huo, Dkt. Alphonce Dotto Massaga alieleza maono ya Kampuni kwa mwaka 2026 na mikakati ya muda mrefu katika kuimarisha uwezo wa kampuni kwa ujumla kupitia ubunifu na uvumbuzi wa maswala yanayohusu biashara na ushauri wa kikodi

Kwa upande mwingine, Dkt. Massaga aliahidi kushirikiana zaidi na wadau mbalimbali ili kuongeza ubora, ufaninisi wa kazi na idadi ya wateja sambamba na kutoa tathimini ya jitihada zilizofanyika mwaka 2025 kupitia ushirikiano baina ya watumishi wa Alpha Associates Tanzania LTD pamoja na wadau wa maswala ya kodi na biashara

wakati wa hotuba yake Dkt. Massaga alifafanua malengo mbalimbali ya mwaka 2026 kwa wafanyakazi likiwemo, ongezeko la wateja katika matawi yote, ushirikiano wa kina na wadau mbalimbali sambamba na matumizi ya teknolojia ya akili unde "AI

"Alpha associates imejipambanua kama kampuni inayotoa huduma bora na zenye uhakika kwa wateja wake huku teknolojia ikitumika kama kichocheo muhimu cha kuongeza ubora na ufanisi wa shughuli za kampuni" Dkt. Alphonce Dotto Massaga, alielezea.

Aidha Mkurugenzi Mtendaji wa Alpha Associates Tanzania LTD aliendelea kuelezea mikakati endelevu ya miaka 25 ijayo mara baada ya kampuni ya Alpha Associates kusherehekea miaka 25 ya utoaji huduma kwa wateja na jamii ya kitanzania kwa kubainisha nia na malengo ya kuongeza Kufungua matawi katika majiji mikuu ya kibiashara nchini Tanzania yakiwemo makao makuu ya nchi Dodoma, mbeya na Zanzibar ndani ya miaka 10 Kupanua huduma katika nchi za EAC (Kenya, Uganda, Rwanda) ndani ya miaka 15.Kuweka mahusiano ya kitaasisi na makampuni makubwa ya kimataifa ya ukaguzi na kodi (kama PwC, Deloitte, EY au KPMG) kama "affiliates" ifikapo mwaka 2035.
Kuanzisha platform ya kidigitali kwa ajiri ya wateja kuweza kufuatilia masuala yao ya kikodi (Client Tax Portal) kwa Kuwekeza katika kwenye matumizi ya akili unde AI & Data Analytics kusaidia wateja kubaini hatari za kodi na fursa za kisheria Kufikia 100% ya michakato ya ndani kuwa "paperless" ifikapo 2040 ,Kuweka mifumo ya uthibiti wa maadili (Ethics and Compliance Framework) Kukuza kizazi kipya cha washauri wa kodi kupitia programu za mafunzo na Kuanzisha "Alpha Tax Academy" ifikapo 2030.

Kuendelea Kujenga mahusiano mazuri na ushirikiano imara na Taasisi za kimataifa na zandani ya nchi kama vile, UN GLOBAL COMPACT, TPSF, TNCC,NEEC, BDS TANZANIA, TKPA,TISEZA,DSE,TATC,TRA,na taasisi za kisheria, fedha na Tasisi za elimu ya chuo na vyuo vikuu . Kutoa michango ya kitaalamu katika uundaji wa sera za kodi nchini Kuendesha mikutano ya kitaifa ya kodi kila mwaka ("Alpha Tax Forum") Kupanua mapato ya kampuni kwa wastani wa 15% kila mwaka.

**DAR ES SALAAM.**



Kwenye picha ni watumishi wa Alpha Associates Tanzania LTD katika mafunzo ya mfumo Jumuishi wa Utawala wa Mapato ya Ndani (IDRAS), yaliondaliwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) jijini Dar es Salaam katika ukumbi wa mikutano wa Mlimani City.

**Alpha yajipanga kutumia mfumo wa IDRAS kikamilifu**

Kuanzia tarehe 15 hadi 17 Januari 2026, wafanyakazi wa Alpha Associates Tanzania LTD tawi la Dar es Salaam walipata nafasi ya kuhudhuria mafunzo ya mfumo Jumuishi wa Utawala wa Mapato ya Ndani (IDRAS),yaliondaliwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) jijini Dar es Salaam katika ukumbi wa mikutano wa Mlimani City.

Mafunzo ya IDRAS yanalenga kujenga uelewa kwa umma namna ya kutumia Mfumo Jumuishi wa Utawala wa Mapato ya Ndani (IDRAS), hasa kwa washauri wa kodi, Makampuni ya Ukaguzi, wafanyabiashara na wadau wa kimkakati katika sekta ya kodi.

Wakizungumza wakati wa kilele cha mafunzo ya IDRAS tarehe 17 Januari 2026, baadhi ya wawakilishi wa Alpha waliahidi kutumia ujuzi walioupata wakati wa mafunzo hayo ya siku 3 kwa ajili ya kuboresha huduma zinazotolewa na Alpha Associates Tanzania LTD.

Zaidi ya hayo, baadhi ya wafanyakazi wa Alpha walipongeza mabadiliko makubwa ya mifumo ya TRA huku wakisifu muonekano angavu na uwezo wa mfumo katika kuhudumia umma.

Mfumo Jumuishi wa Utawala wa Mapato ya Ndani (IDRAS) unatarajiwa kuzinduliwa rasmi tarehe 9/02/2026, ambapo huduma zote zinazohusiana na kodi zitaendeshwa kwa utaratibu kupitia mfumo shirikishi, ambao umeundwa ili kuhudumia umma na mnyororo mzima wa thamani wa tasnia ya kodi.

## TRA mguu sawa kuzindua mfumo wa IDRAS

Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Yusuph Juma Mwenda, amesema Mfumo Jumuishi wa Usimamizi wa Mapato ya Ndani (IDRAS) unaotarajiwa kuzinduliwa tarehe 9/02/2026 utapanua wigo wa kodi na kuhakikisha usawa katika ulipaji wa kodi.

Ameyasema hayo wakati akifungua rasmi mafunzo ya IDRAS kwa washauri na wahasibu wa kodi jijini Dar es Salaam Januari 15, 2026, Kamishna Jenerali Mwenda alisema kuwa TRA imejipanga kuleta maboresho makubwa ya mifumo ya kodi ya ndani kama sehemu ya kuleta mageuzi makubwa katika ukusanyaji wa mapato kwa kuhakikisha usawa katika tathmini za kodi.

Aliongeza kuwa kupitia IDRAS, Mamlaka itaweza kubaini na kudhibiti aina mbalimbali za ukwepaji kodi, kupanua wigo wa kodi kwa kusajili walipakodi wapya, na wakati huo huo kuwezesha na kulinda biashara za walipakodi.

"Kurahisisha biashara za walipakodi ni pamoja na kutunza kumbukumbu zao. IDRAS itakapoanza kufanya kazi, itakuwa suluhu ya kuweka kumbukumbu za biashara za walipakodi, na rekodi hizo zitakuwa salama," alisema Bw. Mwenda.

Kamishna Jenerali Mwenda aliendelea kusema kuwa nia ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mh. Dk Samia Suluhu Hassan, ni kuona mifumo ya taasisi za serikali inaunganishwa ili kuimarisha uwazi na uwajibikaji. TRA inatekeleza hili kwa vitendo kupitia IDRAS, ambayo itaunganishwa na taasisi nyingine za serikali.

Alifafanua kuwa kupitia IDRAS, walipakodi wataweza kutoa risiti za EFD bila kutumia mashine, na pia kupata Hati ya Kulipa Kodi, hatua inayotarajiwa kurahisisha shughuli za biashara.

"IDRAS itakapoanza kufanya kazi, itakuwa na manufaa makubwa kwa walipakodi, kwani wataweza kufuatilia taarifa zao na maombi yoyote waliyowasilisha TRA kupitia mfumo huo, ambao ni muhimu sana, hasa katika kusimamia akaunti ya mlipakodi," alisema Bw. Mwenda.
Kwa upande wake Kamishna wa Kodi ya Ndani Bw.Alfred Mlegi, alisema waliamua kutoa mafunzo hayo kwa washauri wa kodi kabla ya mfumo huo kuanza kutumika ili kuongeza uelewa wa wananchi na uelewa wa walipakodi kuhusu mfumo huo.

Alibainisha kuwa mfumo huo una jumla ya moduli 17, kati ya hizo 15 ziko tayari kuanza kutumika, huku mbili zilizobaki—ukaguzi na uchunguzi—zinaendelea kutengenezwa




**Yusuph Juma Mwenda**
Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)




Wakati huo huo, Mwenyekiti wa Chama cha Washauri wa Kodi Tanzania (TATC), CPA Victoria Soka, alisema mafunzo hayo yatawasaidia kutekeleza vyema majukumu yao ya ushauri katika masuala ya kodi na kuwawezesha wateja wao kutimiza wajibu wao wa kodi kwa urahisi zaidi kupitia mfumo huo.

"IDRAS itarahisisha usimamizi wa ushuru kwetu kama washauri kwa sababu itatoa ufikiaji wa taarifa zote za walipa kodi, na kuwawezesha kupata huduma kutoka popote," alisema Soka.

ALPHA HABARI
Toleo la Januari
*31 januari, 2026*

**KONA YA DAR ES SALAAM**

# kodi ya mapato kwa makampuni na watu binafsi Nchini Tanzania.

*Imeandaliwa na:(Azaria Suleiman Mhasibu |Meneja wa tawi- Dar es salaam, Alpha Associates Tanzania Limited)*



**Utangulizi**

Kodi ya Mapato ni miongoni mwa kodi muhimu zaidi katika mfumo wa kodi Tanzania. Hata hivyo, kwa muda mrefu imekuwa chanzo kikubwa cha migogoro kati ya wafanyabiashara na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA). Migogoro hii mara nyingi haitokani na ulaghai wa walipa kodi, bali hutokana na ukosefu wa uelewa sahihi wa sheria, taratibu na wajibu wa mlipakodi.

Kupitia makala hii, Alpha Habari inalenga kutoa elimu ya kina kwa wafanyabiashara, makampuni na watu binafsi ili waweze:

- Kuelewa Kodi ya Mapato kwa mujibu wa sheria
- Kusimamia makadirio ya kodi (Provisional Tax) ipasavyo
- Kuwasilisha marejesho ya kodi kwa usahihi na kwa wakati
- Kutunza kumbukumbu sahihi za kifedha

Makala hii imeandaliwa kwa kuzingatia mazingira halisi ya biashara nchini Tanzania, kwa lugha inayoeleweka na mifano hai.

**Maana ya kodi ya mapato na sheria husika**

Kodi ya Mapato ni kodi inayotozwa kwenye faida au mapato yanayopatikana na:

- Makampuni (Corporate Income Tax)
- Watu binafsi wanaofanya biashara au kazi za kujitegemea

Kodi hii inasimamiwa chini ya:

- Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332 (Income Tax Act, CAP 332)
- Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura ya 438 (Tax Administration Act)

Kwa mujibu wa sheria hizi, kila mlipakodi anatakiwa:

- Kutangaza mapato yake kwa usahihi
- Kulipa kodi stahiki kwa wakati
- Kutunza kumbukumbu kwa ajili ya uthibitisho

Kodi ya mapato kwa makampuni

Makampuni yote yaliyoanzishwa na kusajiliwa kisheria yanatakiwa kulipa Kodi ya Mapato kwenye faida wanayopata kutokana na biashara zao.

**Kiwango cha Kodi**

Kwa ujumla, kiwango cha Kodi ya Mapato kwa makampuni ni 30% ya faida inayotozwa kodi, isipokuwa kwa makampuni maalum yanayopata motisha za kikodi kwa mujibu wa sheria au mikataba ya uwekezaji.

Mfano Halisi:

Kampuni A imepata mapato ya Tsh 500,000,000 kwa mwaka. Baada ya kutoa gharama halali za biashara, faida inayotozwa kodi ni Tsh 100,000,000.

Kodi ya Mapato itakuwa:

30% × 100,000,000 = Tsh 30,000,000

Ikiwa kampuni haitapanga mapema kodi hii, inaweza kujikuta ikipata mzigo mkubwa wa kifedha mwishoni mwa mwaka.

**Makadirio ya kodi (provisional tax estimates)**

**Maana ya Provisional Tax**

Kwa mujibu wa Kifungu cha 90 cha Sheria ya Kodi ya Mapato, mlipakodi anatakiwa kukadiria mapato ya mwaka husika mapema na kulipa kodi kwa awamu (installments) kabla ya mwisho wa mwaka wa fedha.

*itaendelea ukurasa wa 7.......*

**DAR ES SALAAM.**

## Mawasiliano kuchochea mageuzi chanya ya kampuni ya Alpha

Akizungumza wakati wa mkutano na wadau tarehe 23 Januari 2026 jijini Dar es salaam, Afisa Mawasiliano na Wadau kutoka Alpha Associates Tanzania LTD Peter Mganga, alieleza umuhimu wa matumizi ya akili unde "Artificial Intelligence" (AI) katika kuimarisha mikakati ya Mawasiliano ya Kampuni ya Alpha associates Tanzania LTD kwa ujumla.



**Peter Mganga**
Afisa mawasiliano na wadau

Kwa upande mwingine Peter Mganga amewataka wadau kushirikiana na Alpha Associates Tanzania LTD kwa maslahi mapana ya ujenzi wa Taifa kupitia sekta ya biashara.

"Alpha Associates Tanzania LTD itaendelea kuimarisha ushirikiano na wadau na jamii kama sehemu ya kuleta mashirikiano endelevu"

Zaidi ya hayo, Peter Mganga alieleza jinsi ushirikiano na kujitolea kwa wafanyakazi unavyochangia katika kutengeneza mikakati endelevu ya mawasiliano kwa mwaka 2026.




Peter Mganga aliongeza kuwa kwa mwaka 2026, mtindo wa mawasiliano wa Alpha Associates Tanzania LTD utaendana na maadhimisho ya miaka 25 ya Ushauri wa Kodi, Urasimishaji Biashara, Kliniki ya Biashara, na Warsha kama sehemu ya kusherehekea mafanikio ya kimkakati yaliopatikana katika kipindi cha miaka 25.





**DAR ES SALAAM**

**Dkt. Massaga "Kodi ya kidijitali kukuza uchumi wa Tanzania"**

Tarehe 28 Januari 2026, Mkurugenzi mtendaji wa Alpha Associates Tanzania LTD, Dkt. Alphonce Dotto Massaga, alieleza jinsi kodi ya kidijitali inavyochukua nafasi kubwa katika kukuza uchumi wa Tanzania.

Akizungumza wakati wa mahojiano katika redio ya Malkia Choice Fm, Dkt. Massaga alishauri watengeneza maudhui (Content creators), washawishi mitandaoni (Influencers), na watumiaji wa mitandao ya kijamii kusajiliwa kama walipa kodi kwa minajili ya kukuza uchumi wa Taifa.


Kwa mujibu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Sheria ya Fedha, 2024, ilianzisha vifungu vipya chini ya Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura. 332: Sehemu ya 83B: Huamuru wakazi au wasio wakaazi wanaolipa watayarishaji wa maudhui dijitali wakaazi kuanza kulipa kodi kwa kiwango cha 5%, Sehemu ya 83C: Huamuru wakaazi au wasio wakaazi wanaomiliki majukwaa ya kubadilishana mali ya kidijitali au kuwezesha ubadilishanaji wa mali ya kidijitali au uhamisho wa kuzuilia kodi kwa malipo ya mali ya kidijitali kwa 3% au uhamisho wa mkaazi, (chanzo TRA).

Pia, Sheria ya Fedha, 2024, ilileta ufafanuzi mpya, chini ya kifungu cha 2 cha Kodi ya Ongezeko la Thamani Sura ya 148 (sehemu ya tafsiri), kuhusu "Huduma za Data Mtandaoni."



**Dr. Alphonce Dotto Massaga**
Mkurungenzi Alpha associates Tanzania Ltd

Zaidi ya hayo, Dk. Alphonce Dotto Massaga aliwataka watengeneza maudhui kufika katika ofisi za Alpha Associates Tanzania LTD zilizopo Arusha, Dar es salaam na Mwanza kwa ajili ya kupata elimu zaidi kuhusu kodi ya kidijitali.



kwenye picha ni watangazaji wa Malkia Choice Fm pamoja na Dr. Alphonce Dotto Massaga baada ya mahojiano

## KONA YA DAR ES SALAAM

**Kodi ya makadilio (Provisional Tax) kwa Makampuni.**

Makampuni hulipa Provisional Tax kwa awamu nne (quarterly installments).

Mfano Halisi:

Kampuni B inakadiria kuwa itapata faida ya Tsh 80,000,000 kwa mwaka.

Kodi inayokadiriwa:

30% × 80,000,000 = Tsh 24,000,000

Hii italipwa kwa awamu nne:

Tsh 6,000,000 kila robo mwaka.

Kushindwa kulipa Provisional Tax kwa usahihi husababisha riba na adhabu, hata kama kampuni italipa kodi yote mwisho wa mwaka.

**Uwasilishaji wa kodi (income tax returns)**

wajibu wa kisheria

kwa mujibu wa kifungu cha 91 cha sheria ya kodi ya mapato, kila kampuni na mlipakodi anatakiwa kuwasilisha income tax return ya mwaka ndani ya muda uliowekwa kisheria.

kwa kawaida:

- makampuni: ndani ya miezi 6 baada ya mwisho wa mwaka wa fedha
- biashara kubwa na za kati: zinatakiwa kuwasilisha ritan zilizoandaliwa kwa viwango vya kitaalamu.

**Ulipaji wa kodi kwa biashara kubwa na za kati**

biashara kubwa na za kati zinatarajiwa:

- kuwa na mifumo madhubuti ya uhasibu
- kuandaa hesabu zilizokaguliwa (audited accounts)
- kuwasilisha marejesho sahihi na kwa wakati

makosa madogo ya kihasibu kwa biashara hizi mara nyingi husababisha ukaguzi wa kodi (tax audit) na makadirio makubwa ya kodi.

**Usimamizi wa kumbukumbu za fedha kwa madhumuni ya kodi**

umuhimu wa kumbukumbu

kwa mujibu wa kifungu cha 34 cha sheria ya usimamizi wa kodi, mlipakodi anatakiwa kutunza kumbukumbu za biashara kwa angalau miaka 5.

kumbukumbu hizi ni pamoja na:

- risiti na ankara
- taarifa za benki
- mikataba
- hesabu za mapato na matumizi

mfano halisi:

mfanyabiashara aliyefanyiwa ukaguzi lakini hana kumbukumbu sahihi, TRA inaweza kukadiria mapato kwa kutumia taarifa za benki au makisio ya mauzo, jambo linaloweza kuongeza kodi mara mbili au zaidi ya hali halisi.

**Umuhimu wa elimu ya kikodi kwa kuepuka kadhia za TRA**

elimu sahihi ya kodi humsaidia mlipakodi:

- kupanga mapato na matumizi
- kujua haki na wajibu wake
- kuepuka migogoro isiyo ya lazima
- kuendesha biashara kwa amani na uhakika

migogoro mingi ya kodi ingeepukika kama walipa kodi wangepata elimu mapema kabla ya matatizo kujitokeza.




nafasi ya alpha associates tanzania limited

alpha associates tanzania limited imejikita katika:

- kutoa elimu endelevu ya kodi
- kuwasaidia wafanyabiashara kutii sheria
- kusimamia marejesho ya kodi kwa usahihi
- kupunguza hatari za kikodi kwa wateja

kupitia alpha associates newsletter, tunalenga kufikisha elimu hii kwa umma mpana wa watanzania.

**MAKALA YA ELIMU KWA WAFANYABIASHARA KUHUSU UMUHIMU WA MATUMIZI YA MIFUMO YA KIDIGITAL (IDRAS) KATIKA UTOZAJI NA ULIPAJI WA KODI TANZANIA**

*Jarida Rasmi la Elimu ya Kodi na Biashara – Alpha Associates Tanzania Limited*
*Imeandaliwa na Dr. Alphonce Dotto Massaga*
*Mkurugenzi Mkuu na Mwanzilishi – Alpha Associates Tanzania Limited*
*Mshauri wa Kodi na Masuala ya Biashara Aliyesajiliwa na Kuthibitishwa*

**Utangulizi**

Katika dunia ya sasa inayoendeshwa kwa kasi ya teknolojia, matumizi ya mifumo ya kidigital yamekuwa si hiari bali ni hitaji la msingi katika kuboresha ufanisi wa taasisi za umma na sekta binafsi. Tanzania, kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), imeendelea kuchukua hatua madhubuti za kisera na kiteknolojia kwa lengo la kuhakikisha ukusanyaji wa kodi unakuwa wa haki, uwazi, na unaoendana na maendeleo ya uchumi wa kisasa. Moja ya hatua hizo ni kuanzishwa na kuimarishwa kwa matumizi ya Mfumo wa Kidigital wa IDRAS (Integrated Domestic Revenue Administration System).

Makala hii inalenga kutoa elimu kwa wafanyabiashara na walipakodi juu ya umuhimu wa matumizi ya mfumo wa IDRAS katika kuleta ufanisi chanya kwa mlipakodi na wakusanya kodi, pamoja na kuchambua kwa kina manufaa na madhara yanayoweza kujitokeza endapo mfumo huo hautatumika ipasavyo.

Jitihada za Kamishna wa TRA katika Kuhakikisha Kodi Sahihi Inalipwa

Kamishna Mkuu wa TRA, kwa kushirikiana na Serikali ya Awamu ya Sita, ameendelea kuonesha dhamira ya dhati katika kujenga mfumo wa kodi unaozingatia haki kwa mlipakodi na maslahi mapana ya taifa. Hivyo kupitia mfumo wa IDRAS, unaotarajiwa kuzinduliwa tarehe 9/2/2026, mfumo huu unatarajiwa kuboresha mambo yafuatayo

- Kupunguza makadirio ya kodi yasiyo sahihi (arbitrary assessments)
- Kuimarisha uwazi katika mchakato wa usajili, uwasilishaji wa marejesho (returns), na malipo ya kodi
- Kurahisisha mawasiliano kati ya mlipakodi na TRA
- Kupunguza mianya ya rushwa na makosa ya kibinadamu

Hatua hizi zinadhihirisha dhamira ya TRA kuhakikisha mfanyabiashara analipa kodi stahiki – si zaidi wala si pungufu – kwa mujibu wa sheria na taarifa halisi za biashara.

**Manufaa kwa Mlipakodi Atakayetumia Mfumo wa IDRAS**

Iwapo mfumo huu wa IDRAS utatumika kwa usahihi mfanyabiashsra au mlipa kodi atapata manufaa makubwa yakiwemo:

1. Urahisi na Ufanisi wa KitaalumaMfumo wa IDRAS utamwezesha mlipakodi kuwasilisha marejesho ya kodi, kufanya malipo, na kufuatilia mwenendo wa akaunti yake ya kodi kwa njia ya mtandao bila usumbufu.
2. Kupunguza Adhabu na RibaKwa kuwa mfumo unakumbusha tarehe za mwisho za uwasilishaji na malipo, mlipakodi atapunguza hatari ya kuchelewa na hivyo kuepuka adhabu na riba zisizo za lazima.
3. Uwiano kati ya Mapato na Kodi Inayodaiwa Taarifa halisiza kifedha na biasharazitakazotunzwa kwenye mfumo waIDRAS zitaonyesha uhalisia hivyo kodi itakokotolewa kuendana na uwezo halisi wa biashara.

Madhara ya Kutotumia Mfumo wa IDRAS kwa Mlipakodi

Kinyume chake, kushindwa au kukataa kutumia mfumo wa IDRAS kunaweza kuleta athari zifuatazo:

- Makadirio ya Kodi Yasiyo Sahihi kutokana na ukosefu wa taarifa za kuaminika
- Adhabu na Riba Kubwa kwa kuchelewa au kutowasilisha marejesho
- Migogoro ya Mara kwa Mara na TRA inayopoteza muda na rasilimali
- Hatari ya Kuchukuliwa Hatua za Kisheria ikiwa ni pamoja na kufungiwa biashara au akaunti za benki
- Kudidimia kwa Uaminifu wa Biashara mbele ya taasisi za fedha na wawekezaji

Faida tarajiwa za Matumizi ya IDRAS kwa Upande wa TRA

Kwa upande wa TRA, mfumo wa IDRAS unatarajiwa kuleta mapinduzi makubwa katika ukusanyaji wa mapato ya ndani ikiwa ni pamoja na

- Kuongeza ufanisi wa ukusanyaji wa kodi
- Kupunguza gharama za uendeshaji na utegemezi wa mifumo ya mikono
- Kuimarisha uchambuzi wa data kwa ajili ya kupanga sera bora za kodi
- Kupanua wigo wa walipakodi kwa kutambua biashara zisizosajiliwa

Hatimaye, TRA itaweza kuongeza mapato ya ndani bila kuongeza viwango vya kodi, bali kwa kuboresha mifumo.

Linganisho: Mazingira ya Biashara Zamani na Sasa

Zamani, kabla ya matumizi ya mifumo ya kidigital, wafanyabiashara walikabiliwa na:

- Misururu mirefu ya foleni
- Makosa katika makadirio ya kodi
- Ukosefu wa kumbukumbu sahihi
- Malalamiko mengi dhidi ya TRA

Leo hii, katika mazingira ya kidigital:

- Huduma zinapatikana mtandaoni saa 24
- Uwajibikaji na uwazi umeongezeka
- Mahusiano kati ya mlipakodi na TRA yameimarika
- Biashara zinafanya maamuzi kwa kutumia taarifa sahihi

Mwelekeo wa Dira ya Taifa 2025/2050

Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 na mwelekeo wa 2050 inalenga kujenga uchumi shindani. Matumizi ya mifumo ya kidigital kama IDRAS ni nyenzo muhimu katika:

- Kuongeza mapato ya ndani
- Kupunguza utegemezi wa misaada ya nje
- Kuwezesha Serikali kugharamia huduma za jamii kwa mapato ya ndani

Nafasi ya Alpha Associates Tanzania Limited katika Elimu na Ushauri wa Kodi

- Kuelimisha umma kuhusu wajibu na haki za mlipakodi
- Kusaidia wafanyabiashara kutumia mifumo ya kidigital kama IDRAS ipasavyo
- Kupunguza adhabu, migogoro, na changamoto zisizo za lazima na TRA

Kupitia semina, makala za kielimu, na ushauri binafsi, Alpha Associates itaendelea kuwa mshirika wa maendeleo kati ya Serikali na sekta binafsi.

Hitimisho

Matumizi ya mifumo ya kidigital kama IDRAS si tu yanarahisisha ulipaji wa kodi, bali ni nguzo muhimu katika kujenga uchumi wa kisasa, unaozingatia haki, uwazi, na maendeleo endelevu. Ni wajibu wa kila mfanyabiashara kuchangamkia mifumo hii kwa maslahi yake binafsi na taifa kwa ujumla.

Imetolewa kwa elimu ya umma.

ALPHA HABARI
Toleo la Januari
*31 januari, 2026*

**YAJUE MALENGO NA SHABAHA YA DIRA 2050 NA MBINU ZA KUUFIKIA UCHUMI WA DOLA TRILION 1 IFIKAPO 2050**

*Dkt. Alphonce Dotto Massaga Mkurugenzi wa Alpha Associates Tanzania Limited, washauri wa kodi na biashsra.*

**Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050** ni ramani kabambe ya kuifikisha Tanzania kwenye uchumi wa dola trilioni 1 ifikapo mwaka 2050. Dira hii inalenga kuijenga Tanzania kuwa taifa lenye ustawi wa watu wake, uchumi shindani kimataifa, na matumizi endelevu ya rasilimali, huku teknolojia na umahiri wa watu ukiwa kichocheo kikuu cha maendeleo.

**Malengo Makuu ya Dira 2050**

Dira ya Maendeleo ya taifa ya 2025/2025 imebebwa na malengo makuu manne kama yalivyoainshwa ndani ya dira yenyewe.

**Lengo la Kwanza**, ni kujenga uchumi mseto, stahimilivu, jumuishi na shindani wa kipato cha kati ngazi ya juu. Hili linamaanisha kuimarisha sekta za uzalishaji, kuongeza thamani ya mazao na rasilimali, na kupanua wigo wa mapato kwa ushiriki wa sekta binafsi.

**Lengo la Pili**, ni kuhakikisha maisha bora na ustawi kwa wote, kupitia huduma bora za kijamii, ajira zenye tija, na mazingira rafiki ya kufanya biashara.

**Lengo la Tatu,** ni kuijenga Tanzania kuwa taifa linalohifadhi na kutumia rasilimali za asili kwa ufanisi, uendelevu na tija, sambamba na kuhimili mabadiliko ya tabianchi.

**Lengo la Nne,** ni kuunda jamii yenye umahiri wa teknolojia za kidijitali, inayochochea ubunifu, ujasiriamali na ushindani wa kimataifa, na iwapo malengo haya yatatekelezwa Tanzania itaweza kuufikia uchumi wa dola trillion moja ifikapo 2050 kwa kutmia mbinu zifuatazo

Mbinu za Kufikia Uchumi wa Dola Trilioni 1

Ili kufanikisha malengo hayo, Tanzania inalenga:

1. Ubunifu na teknolojia kwa kuwekeza TEHAMA, R&D na uchumi wa kidijitali;
2. Miundombinu ya kisasa kama bandari, reli, nishati na miji jumuishi;
3. Viwanda na mnyororo wa thamani katika madini, kilimo, gesi na utalii wa kimkakati;
4. Ushirikiano wa sekta binafsi (PPP) na mazingira bora ya biashara;
5. Uwekezaji kwa watu kupitia elimu ya viwango vya kimataifa na ujuzi wa karne ya 21;
6. Uimarishaji wa biashara za kikanda na kimataifa kwa kutumia AfCFTA na ushirikiano wa kibiashara.

Kwa kutumia mbinu hizo sita, Alpha Associates ina nafasi muhimu ya kuharakisha ufanisi wa Dira 2050 kupitia:
(i) kutoa elimu ya biashara na kodi inayochochea ubunifu na teknolojia;
(ii) kusaidia wafanyabiashara kutumia miundombinu ya kisasa kwa ufanisi wa kifedha na kikodi;
(iii) kushauri viwanda na minyororo ya thamani juu ya utiifu wa kodi na kuongeza tija;
(iv) kuimarisha PPP kwa ushauri wa kisheria na kikodi unaovutia uwekezaji;
(v) kuwekeza kwa watu kwa kutoa mafunzo ya vitendo kwa wahitimu wa vyuo vikuu ili kukuza umahiri wa kazi;
(vi) kusaidia biashara kushindana kikanda na kimataifa kwa kufuata mifumo sahihi ya kodi.

Kwa ufasaha na weledi, Alpha Associates husaidia walipa kodi kulipa kodi stahiki, kuepuka adhabu zisizo za lazima, na kujenga utamaduni wa utiifu—nguzo muhimu ya kufikia uchumi wa dola trilioni 1 ifikapo 2050.

*Imeandaliwa na Dkt. Alphonce Dotto Massaga*

KONA YA ARUSHA

# Makosa ya kawaida ya kodi kwa Biashara Ndogo na za Kati na jinsi ya kuyaepuka au kuyakwepa kisheria

*imeandaliwa na:(Naomi MollelMhasibu |Meneja wa tawi- Arusha Alpha associates Tanzania limited)*



**Utangulizi**

Biashara ndogo na za kati (smes) ndizo mhimili mkuu wa uchumi wa tanzania. zimekuwa chanzo kikubwa cha ajira, kipato kwa wananchi na mapato ya serikali. pamoja na umuhimu huo, smes nyingi zimeendelea kukumbwa na changamoto za kikodi ambazo mara nyingi husababisha migogoro na mamlaka ya mapato tanzania (TRA).

ni muhimu kuelewa kuwa migogoro mingi ya kodi kwa smes haitokani na kukwepa kodi kwa makusudi, bali hutokana na:

- ukosefu wa elimu sahihi ya kodi
- kutojua wajibu wa kisheria
- kutozingatia taratibu za usajili na uwasilishaji wa taarifa

kupitia makala hii, Alpha Habari inalenga kutoa elimu ya kina kwa wafanyabiashara wadogo na wa kati ili:

- watambue makosa ya kawaida ya kodi
- wajue jinsi ya kuyaepuka kisheria



**Maana ya Biashara Ndogo na za Kati katika muktadha wa kodi Tanzania**

kwa mujibu wa sera na mifumo ya kodi Tanzania, sme ni biashara ndogo au ya kati kulingana na:

- kiasi cha mtaji
- kiwango cha mauzo ya mwaka
- idadi ya wafanyakazi

TRA imeweka mifumo maalum ya kodi kwa smes ili kurahisisha ulipaji wa kodi, hususan kupitia mfumo wa presumptive tax. hata hivyo, mfumo huu unahitaji uelewa sahihi ili kuepuka matumizi yasiyo sahihi yanayosababisha matatizo ya kikodi.

**1. Kosa la kwanza: Kutokua na namba ya utambulisho ya mlipa kodi. (TIN)**

wajibu wa kisheria wa kusajili biashara

kwa mujibu wa:

- sheria ya usimamizi wa kodi, sura ya 438 (tax administration act)
- sheria ya kodi ya mapato, sura ya 332 (income tax act)

kila mtu anayefanya biashara anatakiwa:

- kusajili biashara yake (BRELA au mamlaka husika)

2. kuomba na kupata namba ya utambulisho wa mlipakodi (TIN)

**umuhimu wa kuwa na TIN**

TIN ndiyo utambulisho rasmi wa mlipakodi mbele ya tra. bila TIN:

- huwezi kuwasilisha marejesho ya kodi
- huwezi kulipa kodi kwa usahihi
- TRA inaweza kukukadiria kodi kwa makisio

mfano halisi

mfanyabiashara wa duka la jumla anaendesha biashara kwa miaka 3 bila kusajili biashara wala kuwa na TIN. TRA inapofanya ufuatiliaji kupitia akaunti za benki au EFD, mfanyabiashara huyu anakadiriwa kodi ya miaka yote kwa makisio, pamoja na adhabu na riba.



**2. Kosa la pili: kutotambua aina ya kodi inayomhusu sme**

kodi kwa smes na wafanyabiashara wadogo

smes nyingi hulipa kodi kupitia mfumo wa:

- presumptive tax (kwa wafanyabiashara wadogo)
- au mfumo wa kawaida wa kodi ya mapato (kwa waliovuka vigezo)

mfumo wa presumptive tax unazingatia mauzo ya mwaka, si faida halisi.

mfano halisi wa presumptive tax

mfanyabiashara mwenye mauzo ya tsh 8,000,000 kwa mwaka anaweza kulipa kodi kwa kiwango kilichowekwa kwenye jedwali la presumptive tax bila kuwasilisha hesabu za kina.

hata hivyo, kama mauzo yanaongezeka hadi Tsh 30,000,000 na mfanyabiashara anaendelea kutumia mfumo wa presumptive bila kubadili, tra inaweza:

- kurekebisha kodi ya nyuma
- kutoza riba na adhabu

**3. Kosa la tatu: kutoelewa kodi za zuio (withholding tax)**

kodi za zuio ndizo chanzo kikubwa cha makosa kwa smes.

maana ya kodi ya zuio

kodi ya zuio ni kodi inayokatwa wakati wa malipo na kuwasilishwa tra kwa niaba ya mlipaji wa mapato. kwa mujibu wa kifungu cha 83 cha sheria ya kodi ya mapato, baadhi ya malipo yanapaswa kukatwa kodi kabla ya kumlipa mhusika.

**Aina za kodi za zuio na mifano halisi**

**(a) Kodi ya zuio kwenye huduma (service fees)**

mfanyabiashara anapolipa:

- fundi
- mshauri
- mkandarasi mdogo

anatakiwa kukata withholding tax kwa kiwango kilichowekwa kisheria.

mfano:

sme inalipa Tsh 1,000,000 kwa fundi wa tehama.

ikiwa kiwango cha zuio ni 5%:

- kodi ya zuio = Tsh 50,000
- fundi analipwa Tsh 950,000
- tsh 50,000 inapelekwa tra

kosa la kawaida: kulipa Tsh 1,000,000 yote bila kukata kodi.

**(b) Kodi ya zuio kwenye kodi ya pango (rental income)**

mfanyabiashara anayekodisha jengo la biashara anatakiwa:

- kukata kodi ya zuio ya pango
- kuiwasilisha tra kila mwezi

mfano:

kodi ya pango = Tsh 2,000,000

kodi ya zuio (10%) = Tsh 200,000

kosa: kulipa pango lote bila kukata kodi, kisha TRA inamdai mpangaji kodi hiyo pamoja na adhabu.

**(c) Kodi ya zuio kwenye malipo ya usambazaji au tume (commission)**

smes nyingi hulipa mawakala au wauzaji kwa mfumo wa tume.

mfano:

mwakala analipwa tume ya Tsh 500,000

kodi ya zuio (5%) = Tsh 25,000

kosa: kutokukata kodi kwa kisingizio kuwa "ni makubaliano binafsi".

**4. kosa la nne: kutokuwa na kumbukumbu sahihi za fedha**

kwa mujibu wa kifungu cha 34 cha sheria ya usimamizi wa kodi, mlipakodi anatakiwa kutunza kumbukumbu kwa angalau miaka 5.

kumbukumbu muhimu ni:

- risiti
- ankara
- taarifa za benki
- mikataba
- rejesta ya mauzo

mfano halisi

sme inapofanyiwa ukaguzi wa kodi bila kumbukumbu sahihi, tra hutumia:

- taarifa za benki
- makadirio ya mauzo

hali hii husababisha kodi kubwa kuliko hali halisi ya biashara.

*itaendelea toleo lijalo.....*

**Jukwaa la uwekezaji na fursa za kiuchumi Nchini**

Tarehe 20/01/2026 Jukwaa la uwekezaji lilifanyika jijini Arusha ambapo lilikutanisha wadau mbalimbali kutoka katika sekta binafsi na Taasisi za umma kwa lengo la kujadili namna wezeshi ya uwekezaji Nchini, Jukwaa la uwekezaji liliandaliwa na Chama cha Wafanyabiashara Tanzania (TNCC) kwa kushirikiana na Mamlaka ya Uwekezaji Tanzania (TISEZA) na Baraza la Biashara la Afrika Mashariki (EABC).



Aidha, mafunzo na mada zilizowasilishwa zilizingatia mahitaji halisi ya wawekezaji wa ndani wadogo na wa kati, kutoa maarifa muhimu kuhusu upatikanaji wa mitaji, masoko, usajili wa miradi, pamoja na fursa za vivutio vya kodi na ulinzi wa kisheria.

Kwa ujumla jukwaa hilo limeonekana kuwa mfano bora wa mikutano ya kimkakati inayochochea uwekezaji, ikiandaliwa kwa ubora, nidhamu na mwelekeo unaokidhi mahitaji ya wawekezaji wa ndani, huku udhamini wa Benki ya Rasilimali Tanzania (TIB) na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) ukiimarisha zaidi mafanikio na heshima ya mkutano huo.

Katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2025/26 (Julai–Septemba 2025), TISEZA imesajili jumla ya miradi 201 yenye thamani ya zaidi ya dola milioni 2,538.56 za Marekani, sawa na shilingi trilioni 6.18 za Kitanzania, ikitarajiwa kuleta ajira zaidi ya 20,800 kwa Watanzania (chanzo TISEZA)



TISEZA imesajili miradi minane (8) yenye thamani ya dola milioni 97.83, ikitarajiwa kutoa ajira kwa zaidi ya watu 2,600 na kuingiza nchi mapato ya fedha za kigeni ya takribani dola milioni 127.53.

Ikilinganishwa na miradi mitatu tu iliyosajiliwa mwaka uliopita, ongezeko hili linaashiria kuimarika kwa mazingira ya biashara na kuongezeka kwa imani ya wawekezaji katika soko la Tanzania



Tanzania ni miongoni mwa nchi 10 za Afrika zinazokua kwa kasi kiuchumi. Kwa miaka 10 iliyopita, uchumi wa nchi ulikua kwa wastani wa asilimia 7. Mnamo Julai 2020, Tanzania ilipandishwa rasmi na kuwa nchi ya uchumi wa kipato cha mwanzo cha kati na Benki ya Dunia. Mafanikio haya yanaweza kuhusishwa na utulivu wa kisiasa na kiuchumi, sera nzuri na zinazotabirika pamoja na amani na utulivu.

KONA YA MWANZA

# ijue kodi ya ongezeko la thamani (VAT) kwa undani zaidi nchini tanzania

*Imeandaliwa na: (Lucas MabulaMhasibu|Meneja wa tawi - Mwanza- Alpha Associates Tanzania Limited)*



**Utangulizi**

Kodi ya Ongezeko la Thamani (Value Added Tax – VAT) ni miongoni mwa kodi zinazokusanywa kwa kiwango kikubwa nchini Tanzania. Pamoja na umuhimu wake, VAT imekuwa chanzo kikuu cha migogoro kati ya wafanyabiashara na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), hasa kwa wafanyabiashara wasiokuwa na uelewa wa kutosha kuhusu:

- Nani anatakiwa kujiandikisha VAT
- Nani hatakiwi kujiunga na VAT
- Namna ya kukusanya na kuwasilisha VAT
- Athari za makosa ya VAT

Makosa ya VAT mara nyingi husababisha makadirio makubwa ya kodi, adhabu, riba na hata kufungiwa kwa biashara. Kupitia makala hii, Alpha Associates Newsletter inalenga kutoa elimu ya kina, sahihi na ya vitendo ili wafanyabiashara na walipa kodi waweze kusimamia VAT kwa ufanisi na kuepuka misuguano na TRA.




*itaendelea toleo lijalo.....*

**Maana ya VAT na sheria husika**

VAT ni kodi inayotozwa kwenye:

- Uuzaji wa bidhaa
- Utoaji wa huduma
- Uingizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi

VAT inasimamiwa chini ya:

- Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148 (VAT Act, CAP 148)
- Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura ya 438 (Tax Administration Act)

Kwa mujibu wa sheria hizi, VAT ni kodi inayobebwa na mlaji wa mwisho, lakini hukusanywa na mfanyabiashara aliyesajiliwa VAT kwa niaba ya serikali.

**1. nani anatakiwa kujisajili na kukusanya VAT**

Kigezo Kikuu cha Usajili wa VAT

Kwa mujibu wa Kifungu cha 49 cha Sheria ya VAT, mtu au biashara anatakiwa kujiandikisha VAT endapo:

- Mauzo yake ya mwaka yanazidi au yanatarajiwa kuzidi kizingiti cha kisheria (VAT registration threshold)
- Anajihusisha na biashara zinazotozwa VAT (taxable supplies)

**2. utaratibu wa kujiunga na VAT**

Hatua za Kisheria za Usajili wa VAT

Mfanyabiashara anatakiwa:

1. Kuwa na TIN
2. Kuomba usajili wa VAT kupitia mfumo wa TRA (au ofisi husika)
3. Kuwasilisha nyaraka muhimu kama:
   - Leseni ya biashara
   - Mikataba ya upangaji (kama ipo)
   - Taarifa za benki
4. Kufanyiwa uhakiki na TRA
5. Kupata Cheti cha Usajili wa VAT

Baada ya kusajiliwa, mfanyabiashara:

- Anatakiwa kuanza kukusanya VAT mara moja
- Anatakiwa kutumia EFD/EFDMS kutoa risiti za VAT

Mfano Halisi

Kampuni ya usafirishaji inajiandikisha VAT mwezi Machi. Kuanzia tarehe ya usajili, kila anapotoa ankara au risiti, anatakiwa:

- Kutoza VAT
- Kuionyesha VAT wazi kwenye ankara

# NEEC KUBORESHA MAZINGIRA WEZESHI KWA WAJASIRIAMALI VIJANA

Tarehe 7/01/2026 Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC) kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu limevitaka vituo atamizi na vituo vya ubunifu nchini kuwasaidia vijana wabunifu, wajasiriamali na kampuni changa kufahamu sheria za nchi pamoja na taratibu zake ili waweze kukuza biashara zao na kuchangia uchumi wa taifa.

Kwa upande wake, Naibu Mkuu wa Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA) anayeshughulikia Fedha, Mipango na Utawala, Dkt. Eliakira Nnko, amesema kuwa taasisi za elimu zina wajibu mkubwa wa kuandaa mazingira rafiki kwa wanafunzi na vijana ili kuendeleza ubunifu na ujasiriamali, sambamba na kuwajengea uwezo wa kisheria na kiutawala.



Akizungumza wakati wa ziara ya vituo atamizi na ubunifu jijini Arusha Katibu Mtendaji wa NEEC, CPA Beng'i Issa, amesema kuwa vijana wengi wana mawazo mazuri ya biashara lakini hukwama kutokana na kukosa uelewa wa masuala ya kisheria, usajili wa biashara pamoja na mifumo ya kifedha. CPA Beng'i Issa ameongeza kuwa baraza hilo limezindua Mwongozo wa Maendeleo ya Biashara, unaoelekeza namna bora ya kuendesha vituo vya uwezeshaji ili viweze kutoa tija na msaada wa moja kwa moja kwa wajasiriamali na wabunifu chipukizi.

Hayo yamejiri katika Ziara ya Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC) CPA. Beng'i Issa katika Vituo vya Ubunifu na Uendelezaji wa Biashara



ALPHA HABARI
Toleo la Januari
*31 januari, 2026*

KONA YA SHERIA ZA KODI

# Zijue, haki na wajibu wa mlipa kodi chini ya sheria za kodi nchini tanzania

*Imeandaliwa na: (Deogratias A. Massaga Mwanasheria Alpha Associates Tanzania Limited)*



**Utangulizi**

Kodi ni uti wa mgongo wa maendeleo ya taifa lolote. Kupitia kodi, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hupata rasilimali za kugharamia huduma za jamii kama vile elimu, afya, miundombinu, ulinzi na usalama. Pamoja na umuhimu wake, masuala ya kodi yamekuwa chanzo kikubwa cha migogoro kati ya Wafanya Biashara (Walipa Kodi) na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), hasa pale ambapo walipa kodi hawana uelewa wa kutosha juu ya haki zao, wajibu wao na taratibu za kisheria zinazohusu kodi.

Makala hii inalenga kutoa elimu ya kina na endelevu kwa umma wa Watanzania,hususan wafanyabiashara na walipa kodi, ili kuwajengea uelewa mpana wa masuala ya kodi, kuwasaidia kutekeleza wajibu wao kwa hiari na kuepuka misuguano isiyo ya lazima na TRA. Makala inajikita katika kueleza haki na wajibu wa mlipa kodi, makosa ya kikodi na athari zake, nafasi ya mikataba ya kibiashara katika kodi, pamoja na usimamizi wa migogoro ya kodi, pingamizi na rufaa chini ya sheria za kodi nchini Tanzania.

## 1. Haki na Wajibu wa Mlipa Kodi Chini ya Sheria za Kodi

### 1.1 Wajibu wa Mlipa Kodi

Chini ya Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura ya 438 (Tax Administration Act, Cap. 438 R.E. 2019), kila mlipa kodi ana wajibu wa:

- Kujisajili kwa ajili ya kodi husika (TIN, VAT, PAYE n.k.) kwa wakati unaotakiwa kisheria.
- Kuwasilisha marejesho ya kodi (tax returns) kwa usahihi na kwa wakati.
- Kulipa kodi stahiki kwa mujibu wa sheria bila kuchelewa.
- Kuhifadhi kumbukumbu za kifedha kwa kipindi kisichopungua miaka mitano (5) kama inavyoelekezwa chini ya Kifungu cha 36 cha Tax Administration Act.
- Kutoa ushirikiano kwa TRA wakati wa ukaguzi wa kodi (tax audit) au uchunguzi (tax investigation).

Mfano Halisi:

Mfanyabiashara anayejihusisha na uuzaji wa vifaa vya ujenzi jijini Dar es Salaam, endapo mauzo yake ya mwaka yanazidi kiwango kilichowekwa kisheria (kwa sasa Tsh 100,000,000),

### 1.2 Haki za Mlipa Kodi

Pamoja na wajibu, sheria pia zimetoa haki mahsusi kwa walipa kodi, zikiwemo:

- Haki ya kutendewa kwa haki na kwa mujibu wa sheria.
- Haki ya kupata taarifa sahihi na kwa wakati kutoka TRA.
- Haki ya kupinga makadirio ya kodi endapo hayaridhishi.
- Haki ya kukata rufaa dhidi ya maamuzi ya TRA.
- Haki ya usiri wa taarifa za mlipa kodi kama inavyolindwa chini ya Kifungu cha 22 cha Tax Administration Act.

## 2. Makosa ya Kikodi na Athari Zake Kisheria kwa Mlipa Kodi

### 2.1 Aina za Makosa ya Kikodi

Makosa ya kikodi yanaweza kufanywa kwa makusudi au kwa kutojua. Baadhi ya makosa ya kawaida ni:

1. Kushindwa kuwasilisha marejesho ya kodi kwa wakati.
2. Kutoa taarifa za uongo au kupunguza mapato kimakusudi (tax evasion).
3. Kutotumia au kuchezea mashine za EFD kinyume na Kanuni za EFD.

**2.2 Athari za Kisheria**

Chini ya Tax Administration Act, makosa ya kikodi yanaweza kusababisha:

- Adhabu (penalties) – mfano adhabu ya kuchelewesha kuwasilisha marejesho.
- Riba (interest) juu ya kodi iliyocheleweshwa kulipwa.
- Makadirio ya kodi kwa nguvu (jeopardy assessment).
- Mashtaka ya jinai, hasa pale kunapothibitika nia ya kukwepa kodi.

Mfano Halisi:

Kampuni iliyoshindwa kuwasilisha marejesho ya kodi ya mapato kwa miaka miwili mfululizo inaweza kukadiriwa kodi na TRA bila kusikilizwa, na kutozwa adhabu pamoja na riba, jambo ambalo linaweza kuathiri mtiririko wa fedha (cash flow) wa biashara husika



**3. Mikataba ya Kibiashara na Athari Zake Kwenye Masuala ya Kodi**

Mikataba ya kibiashara ina mchango mkubwa katika masuala ya kodi. Chini ya Sheria ya Mikataba, Sura ya 345 (Law of Contract Act), mkataba halali una athari za kisheria kwa pande zote.

3.1 Athari za Kodi Katika Mikataba

- Kodi ya Zuio (Withholding Tax) – mikataba ya huduma, ushauri, ujenzi n.k.

2. VAT kwenye mikataba ya huduma na bidhaa.
3. Kodi ya mapato ya kampuni au mtu binafsi.

**4. Usimamizi wa Migogoro ya Kodi kati ya Mlipa Kodi na TRA**

Migogoro ya kodi ni jambo la kawaida katika utekelezaji wa sheria za kodi. Migogoro inaweza kutokea wakati wa:

- Ukaguzi wa kodi (Tax Audit)
- Uchunguzi wa kodi (Tax Investigation)
- Makadirio ya kodi

Sheria inahimiza usuluhishi wa awali kwa njia ya majadiliano (amicable settlement) kabla ya kuingia kwenye hatua za kisheria.

**5. Pingamizi na Rufaa za Kodi (Tax Objections and Appeals)**

**5.1 Pingamizi (Tax Objection)**

Chini ya Kifungu cha 51 cha Tax Administration Act, mlipa kodi ana haki ya kuwasilisha pingamizi dhidi ya makadirio ya kodi ndani ya siku 30 tangu tarehe ya notisi ya makadirio.

Masharti muhimu ya pingamizi ni:

- Kuandikwa kwa maandishi
- Kutoa sababu za pingamizi
- Kulipa kodi isiyopingwa au kuomba msamaha (waiver)

**5.2 Rufaa (Tax Appeal)**

Endapo mlipa kodi haridhishwi na uamuzi wa Kamishna wa TRA, ana haki ya kukata rufaa kwenye Bodi ya Rufaa ya Kodi (Tax Revenue Appeals Board) na baadaye Baraza la Rufaa ya Kodi (Tax Revenue Appeals Tribunal).

Mfano Halisi:

Mfanyabiashara aliyekadiriwa kodi kubwa kutokana na makosa ya ukokotoaji anaweza kuwasilisha pingamizi, na endapo halitazingatiwa ipasavyo, kukata rufaa ili kulinda haki zake.

**Hitimisho**

Uelewa sahihi wa haki na wajibu wa mlipa kodi ni msingi wa mahusiano bora kati ya walipa kodi na TRA. Elimu ya kodi si jukumu la Serikali pekee bali ni wajibu wa kila mdau kuhakikisha anazingatia sheria, anajua haki zake na anatumia njia sahihi za kisheria kutatua migogoro ya kodi.



*itaendelea toleo lijalo.....*

## KONA YA MASWALI KWA WASOMAJI

**Swali la 1**
Kodi ya Mapato nchini Tanzania inasimamiwa chini ya sheria zipi kuu?
A. VAT Act na Excise Act
B. Income Tax Act CAP 332 na Tax Administration Act CAP 438
C. Companies Act na Banking Act
D. TRA Act pekee

**Swali la 2**
Kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Kodi, mlipakodi anatakiwa kutunza kumbukumbu za kifedha kwa muda wa miaka mingapi?

**Swali la 3**
Chanzo kikuu cha migogoro ya kodi kwa SMEs nyingi, kama ilivyoelezwa kwenye makala, ni kipi?
A. Kukwepa kodi kwa makusudi
B. Viwango vikubwa vya kodi
C. Ukosefu wa elimu sahihi ya kodi
D. Ukaguzi wa TRA

**Swali la 4**
SME imelipa fundi Tsh 1,000,000 kwa huduma, kiwango cha Kodi ya Zuio ni 5%. Kodi ya Zuio ni kiasi gani?

**Swali la 5**
Ni sheria ipi inayosimamia wajibu na haki za mlipa kodi kwa ujumla nchini Tanzania?
A. VAT Act, Cap. 148
B. Income Tax Act, Cap. 332
C. Tax Administration Act, Cap. 438
D. Law of Contract Act, Cap. 345

**Swali la 6**
Kwa nini mikataba ya kibiashara ni muhimu katika masuala ya kodi?

**Swali la 7**
IDRAS inasimama kwa maana ipi?
A. Integrated Digital Revenue Accounting System
B. Integrated Domestic Revenue Administration System
C. Internal Digital Revenue Assessment System
D. Integrated Data Reporting and Analysis System

**Swali la 8**
Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) ni kodi inayotozwa kwenye mambo yapi?
A. Faida ya biashara pekee
B. Mishahara ya wafanyakazi
C. Uuzaji wa bidhaa, utoaji wa huduma na uingizaji wa bidhaa
D. Mauzo ya ndani pekee


**Swali la 9**
Mfanyabiashara amekusanya VAT ya Tsh 3,000,000 na amelipa VAT ya Tsh 1,200,000 kwa wasambazaji. VAT ya kulipa TRA ni kiasi gani?

**Swali la 10**
Kwa maoni yako, kwa nini matumizi ya mifumo ya kidigital kama IDRAS ni muhimu katika kufikia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025/2050?

- Walengwa wa maswali haya na wanao takiwa kujibu ni wanafunzi wa vyuo vikuu na wafanyabiashara
- Majibu yote yatumwe kupitia barua pepe md@alphaassociates.co.tz au nambari ya whatsaap 0768449886.
- Watakao jibu vyema na kwa usahihi watapata zawadi
- Jibu Maswali yote 10 ili ujihakikishie ushindi
- Washindi watano watapewa zawadi na kutatangazwa katika toleo la Februari
- Mwisho wa kutuma/kuwasilisha majibu ni tarehe 20/2/2026.

kwa msaada/ maelezo zaidi tupigie 0768449886.
Vigezo na masharti kuzingatiwa.

# KUHUSU ALPHA ASSOCIATES TANZANIA LIMITED



Dkt. Alphonce Dotto Massaga - Mkurungenzi Alpha associates Tanzania Ltd

Alpha Associates ilianzishwa chini ya uongozi na dira ya kitaaluma ya Dkt. Alphonce Dotto Massaga, mtaalamu bingwa wa masuala ya kodi, uhasibu, usimamizi wa biashara na maendeleo ya sera za kiuchumi. Kama mwanzilishi na Mkurugenzi Mkuu, Dkt. Massaga ameiongoza Alpha Associates kwa misingi ya weledi, uzalendo na dhamira ya dhati ya kuelimisha na kuinua uwezo wa wafanyabiashara wa Kitanzania.

Kupitia uzoefu wake mpana wa kitaaluma na kiutendaji, Dkt. Alphonce Dotto Massaga ameweka mkazo mkubwa katika utoaji wa elimu ya kodi na biashara kwa lugha rahisi, inayoeleweka na inayolenga vitendo, ili kuwasaidia walipa kodi kutimiza wajibu wao kwa hiari na kwa usahihi.

Dira yake imekuwa ni kuifanya Alpha Associates kuwa kituo cha maarifa kinachounganisha nadharia na vitendo katika masuala ya kodi, uhasibu na usimamizi wa biashara.

Chini ya uongozi wake, Alpha Associates imejijengea heshima kama mshirika wa kuaminika kwa wafanyabiashara wadogo na wa kati, makampuni yanayokua, taasisi za serikali, pamoja na vyuo vikuu kupitia programu ya mafunzo ya vitendo kazini kwa wahitimu wa vyuo vikuu wanaohitaji mwongozo wa kitaaluma.

kupitia Dkt. Massaga kampuni ya Alpha Associates Tanzania limited imekua nguzo muhimu katika kujenga kizazi cha wataalamu wenye umahiri wa kazi, kwa kuanzisha na kusimamia programu za mafunzo ya vitendo, ushauri elekezi (mentorship) na malezi ya kitaaluma kwa vijana.

Kwa jumla, mchango wa Dkt. Alphonce Dotto Massaga kama mwanzilishi na Mkurugenzi Mkuu umeifanya Alpha Associates kuwa taasisi yenye mchango wa moja kwa moja katika kujenga uchumi shindani, walipa kodi waadilifu, na maendeleo endelevu ya biashara nchini Tanzania. Kupitia uongozi wake, Alpha Associates inaendelea kuwa chombo muhimu cha kufanikisha ajenda ya maendeleo ya Taifa na ustawi wa Watanzania.

Arusha, Golden Rose Conference Centre Arcade, 2nd Floor
P.O.BOX 1863, Arusha, Tanzania
Mwanza, Nyanza Cooperative Union Building 3rd Floor
Dar es salaam, Samora Avenue,
Acacia Building 119/49, 4th Floor
P.O.BOX 22366, Dar es Salaam, Tanzania

Arusha - Tel: +255 742 449 88
Dar es Salaam - Tel: +255 768 488
Mwanza - Tel: +255 747 449 88
ww.alphaassociates.co.tz
info@alphaassociates.co.tz
md@alphaassociates.co.tz / peter@alphaassociates.co.tz